

WABOBEZI WAKUTANA KWA RIPOTI YA PILI YA APRM

Wabobezi katika masuala mbali mbali nchini (Technical Assessment Team) wameombwa kuwa tayari kuanza mchakato wa kufanya tathmini ya pili ya Utawala Bora Nchini ambapo itahusisha maeneo Demokrasia na Utawala wa Kisiasa, Usimamizi wa Uchumi, Utendaji wa Mashirika ya biashara na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi.



Hayo jamesemwa na Bw. Lamau Mpolo ambaye ni Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Mpango wa hiyari wa kujipima kwa vigezo vya Utawala Bora (APRM Tanzania) katika mkutano wa wadau uliofanyika katika Ofisi za APRM jinini Dar-es-Salaam.

Bw. Lamau amesema kuwa lengo kuu la mkutano huo ni kukusanya mawazo ya wadau na kupanga mipango Bora ya kuweza ya kuweza kufanya Ripoti hiyo ya pili ya Utawala Bora kwa haraka na mafanikio makubwa.

Kwa Upande wake Mkurugenzi wa REPOA Dkt. Lucas Katera amesema kuwa kwa vile Tanzania sio kisiwa hivyo inapaswa kujitathmini katika masuala ya Utawala Bora na kujilinganisha na nchi nyengine za Bara la Afrika.

Ameongeza kuwa, Ripoti ya kwanza iliyoifanyika na kusifiwa Barani Afrika Serikali iliweza kupambanua changamoto zilizopo na njia gani Bora za kuzitatua.

Nae Mratibu wa masuala ya Maendeleo ya Jamii APRM Tanzania Balozi Hemed Mgaza ameeleza kuwa katika lolote linalofanyika ni vyema kufanya tathmini ili kutambua mazuri na mabaya yaliopp na njia Bora za kufanya maboresho ambalo ndio lengo kuu la uwepo wa APRM.



Bw. Lamau Mpolo
Katibu Mtendaji - APRM Tanzania

